



Hakika muumini peponi atakuwa na Hema moja la madini ya lulu lililo wazi urefu wake kwenda juu ni maili sitini, muumini humo atakuwa na wake, akiwazungukia na wala baadhi yao hawawaoni wenzao

Kutoka kwa Abuu Musa radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume rehema na amani za Allah ziwe juu yake, amesema: "Hakika muumini peponi atakuwa na Hema moja la madini ya lulu lililo wazi urefu wake kwenda juu ni maili sitini, muumini humo atakuwa na wake, akiwazungukia na wala baadhi yao hawawaoni wenzao".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake baadhi ya neema za peponi, nakwamba muumini ndani ya pepo atakuwa na hema pana kwa ndani, lilitokana na madini ya lulu yenye kung'aa, upana wake na urefu wake kuelekea juu ni maili sitini, katika kila mahali na kila kona katika kona zake nne kuna wake, na wote hawaonani, muumini atakuwa akiwazungukia.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/8349>

